

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI

31 MEI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI – TAREHE 31 MEI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu

utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

331. MHESHIMIWA SANTIEL ERIC KIRUMBA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuunganisha Mifuko ya Mikopo iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ili kuwezesha makundi maalum kupatiwa Mikopo kwa urahisi zaidi.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

332. MHESHIMIWA JAFARI WAMBURA CHEGE (RORYA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Hospitali ya Wilaya ya Rorya itaanza kutoa huduma.

**333. MHESHIMIWA SILLO DANIEL
BARAN (BABATI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi,
Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo
cha Afya Bashnet baada ya Serikali ya
Kijiji kutenga eneo kwa ajili ya ujenzi huo.

**334. MHESHIMIWA FRANCIS KUMBA
NDULANE (KILWA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi,
Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa
kupeleka Watumishi wa Idara ya Afya
katika Jimbo la Kilwa Kaskazini ambalo
lina uhaba wa Watumishi hali
inayopelekea baadhi ya Zahanati kutoa
huduma duni.

**335. MHESHIMIWA REGINA NDEGE
QWARAY (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi,
Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapeleka na kuongeza
Vifaa tiba na Wataalam katika Vituo vya
Afya vilivyojengwa ikiwemo; vifaa tiba
maalumu kama vile *incubator beds* na taa

maalumu kwa ajili ya kukabiliana na Homa ya Manjano kwa Watoto Njiti.

WIZARA YA KILIMO:

336. MHESHIMIWA NUSRAT SHAABAN HANJE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia Mashamba ya uzalishaji mbegu kutatua tatizo la upatikanaji wa Mbegu bora hususan za Alizeti ambayo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa Mkoa wa Singida.

WIZARA YA MAJI:

337. MHESHIMIWA DKT. JASSON SAMSON RWEIKIZA (BUKOBA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

- (a) Je, ni lini ujenzi wa Mradi wa Maji katika Kata za Izimbya, Kyaitoke, Ruhunga, Mugajwale, Katoro na Kaibanja utaanza na kukamilika;
- (b) Je, ni lini Mradi wa maji wa Kata za Kemondo, Katerero na Bujugo utaanza na kukamilika;

- (c) Je, ni lini Mradi wa Maji wa Kata za Karabagaine, Maruku na Kanyangereko utaanza na kukamilika.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

338. MHESHIMIWA JACKSON GEDION KISWAGA (KALENGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, ni lini Serikali itawafanya Wabunge kuwa Wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi kutokana na ukweli kwamba wao hupelekewa migogoro mingi ya ardhi na mashamba.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

339. MHESHIMIWA MINZA SIMON MJIKA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Barabara ya kutoka Kolandoto hadi Meatu itajengwa kwa kiwango cha Lami.

**340. MHESHIMIWA MARIAM DITOPILE
MZUZURI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Nyumba za Viongozi Waandamizi wa Serikali kama Makatibu Wakuu na Mawaziri katika Mji wa Dodoma kwa ajili ya Makazi ya Viongozi hao.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**DODOMA
31 MEI, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**